TANGAZO LA SERIKALI Na. 869 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA YA MWAKA 2024

Jina

TS Na. 221 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6 (1) kwa kufuta maneno "kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni" na badala yake kuweka maneno "saa ishirini na nne kwa siku".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu ya Tano, kwa kuongeza neno "binafsi" mara baada ya neno "Kampuni" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 6;

(b) kwa kufuta Sehemu ya Saba;

(c) katika Sehemu ya Kumi na Moja, kwa-

(i) kufuta maneno "36,000/=, Kwa Mwezi 3000/=" yaliyopo katika safu ya tatu ya kipengele cha 4 na badala yake kuweka maneno "36,000/= Kwa Mwaka, 3000/= Kwa Mwezi"; na

(ii) kufuta kiasi "3000,000/=" kilichopo katika safu ya tatu ya kipengele cha 6 na badala yake kuweka kiasi "300,000/="; na

(d) kwa kubadili mpangilio wa Sehemu ya Nane hadi Ishirini na Nane na kuwa Sehemu ya Saba hadi Ishirini na Saba mtawalia.

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*